


Niliwasili katika kituo chetu cha basi. Kilikuwa kimejaa watu.




Kondakta wa basi aliita, "Kwenda jijini! Tunaondoka sasa!"



Watu walifanya haraka kuingia ndani ya basi.




Wanawake
waliokuwa na
watoto waliketi.
Safari itakuwa
ndefu.



Niliketi kwenye
dirisha karibu na
mwanamume na
mwanamke.



Niliwaza, "Ninaenda
jijini! Nitakosa
familia yangu."



Wachuuzi wengi waliingia kuuza bidhaa zao.




Baadhi ya abiria
walinunua bidhaa.
Sikuwa na pesa ya
kununua chochote.



Ghafla, dereva
alipiga honi.
Tulikuwa tayari
kuondoka.




Wachuuzi
walisukumana
kutoka nje.



"Tutafika saa ngapi?" Nilijiuliza.




Ndani ya basi
mlikuwa na joto
sana.
Niliyafumba macho
yangu.



Niliwafikiri mama na ndugu yangu wakiwa nyumbani.



Baadaye, nilipatwa
na usingizi.



Baada ya muda mrefu, niliamka. Karibu kila abiria alikuwa ameshuka.



Nilianza kutafuta mahali mjomba aliishi.